



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA  
KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO  
WA UBUNGE WA JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA  
KATA SITA ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Mbarali na Madiwani katika kata sita za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023 katika Jimbo la Mbarali na kata sita ambazo ni: -

Na.	Kata	Halmashauri
1.	Nala	Jiji la Dodoma
2.	Mfaranyaki	Manispaa ya Songea
3.	Old Moshi Magharibi	Wilaya ya Moshi
4.	Marangu Kitowo	Wilaya ya Rombo
5.	Mtyangimbole	Wilaya ya Madaba
6.	Mwaniko	Wilaya ya Misungwi

Kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 na kanuni ya 3 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchi nzima, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi mdogo wa Ubunge Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya barua pepe: [info@nec.go.tz](mailto:info@nec.go.tz) au [uchaguzi@nec.go.tz](mailto:uchaguzi@nec.go.tz) Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 5 hadi 12 Agosti, 2023.

Barua ya maombi inatakiwa kuainisha mambo yafuatayo kuhusu taasisi na asasi husika:-


- i. Iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
- ii. Iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
- iii. Ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;
- iv. Katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
- v. Iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
- vi. Iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, maombi hayo yanatakiwa kuambathishwa na: -

- i. Nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
- ii. Nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;
- iii. Majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia;
- iv. Anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake; na
- v. Ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika.

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi na asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

Limetolewa leo tarehe 5 Agosti, 2023 na:

  
Kailima, R. K.  
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**